



NAETISL

National Association of
Educational Translators and
Interpreters of Spoken Languages



MODDC

Missouri
Developmental
Disabilities Council

Kuelewa kategoria za Ulemavu: Mwongozo wa Mzazi

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



naetisl@gmail.com

NAETISL



Follow us



MODDC



moddc@moddcouncil.org



www.naetisl.org

www.moddcouncil.org





Kuelewa kategoria za Ulemavu: Mwongozo wa Mzazi

Kategoria za ulemavu katika elimu maalum ni nini?

Kategoria za Ulemavu ni uainishaji unaotumiwa na shule ili kubaini ikiwa mtoto anastahiki huduma za elimu maalum chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (IDEA). Kategoria hizi husaidia shule kuelewa mahitaji ya kipekee ya mtoto ili kuunda Mpango wa Elimu ya Mtu Binafsi (IEP) ili kusaidia ujifunzaji na maendeleo yake.

Mtoto lazima afikie vigezo vya kategoria moja au zaidi na kuhitaji mafunzo maalum ili afuzu kuwa na IEP. Kuna kategoria 13, kila moja ikiwa na vigezo maalum.

Hii ni orodha ya kategoria hizo na baadhi ya sifa zao:

Usonji

- Unaadhiri mawasiliano, mwingiliano wa kijamii, na tabia
- Unaweza kujumuisha tabia za kujirudilia, hamu kidogo, au changamoto za mabadiliko
- Mara nyingi dalili hujitokeza kabla ya miaka 3

Viziwi-Upofu

- Mchanganyiko nadra wa kupoteza uwezo wa kusikia na kuona
- Husababisha shida kubwa sana ya mawasiliano na kujifunza
- Huhitaji usaidizi katika shughuli za kila siku na maelekezo maalum

Uziwi

- Ulemavu mkubwa sana unaosababisha kuelewa lugha ya mazungumzo kuwa vigumu sana, hata kwa msaada
- Unaweza kuathiri mawasiliano, ukuzaji wa lugha ya mazungumzo, na maendeleo ya kitaaluma





- Mara nyingi huhitaji lugha ya ishara, maelezo mafupi, au usaidizi mwingine

Usumbufu wa Kihisia

- Unajumuisha shida za kiafya kama vile wasiwasi, unyogovu, ugonjwa wa bipolar, au matatizo ya tabia
- Unaweza kujitokeza kama mahusiano mabaya, tabia mbaya, au shida kukabiliana shuleni
- Athiri za kujifunza si kutokana na uwezo wa kiakili

Ulemavu wa Kusikia

- Upotevu wa kusikia wa sehemu au unaobadilika-badilika (sio mbaya kama uziwi)
- Unweza kuathiri kusikiza, ujuzi wa lugha ya kuongea, na ushiriki wa darasani
- Mara nyingi husaidika na visaidizi vya kusikia au mifumo ya kurekebisha masafa, yaani, (FM) systems

Ulemavu wa Kiakili

- Utenda kazi wa chini wa wastani (IQ) na ugumu wa ujuzi wa maisha ya kila siku
- Ujifunzaji wa dhana mpya na kutatua matatizo unaweza kuchukua muda zaidi
- Unaweza kuhitaji maelekezo ya ana kwa ana na mafunzi ya stadi za maisha
-

Ulemavu Mwingi

- Lemavu mbili au zaidi (k.m., Ulemavu wa kiakili na uharibifu wa mifupa)





- Zinasababisha mahitaji makubwa ya kielimu. Mahitaji ni makubwa sana na hayawezi kutatuliwa na huduma za ulemavu mmoja pekee

Uharibifu wa Mifupa

- Ulemavu wa mwili unaoathiri harakati, utaratibu, na nguvu
- Unweza kusababisha hali kama ugonjwa wa kupooza kwa ubongo, mathara kwa uti wa mgongo, au kukatwa viungo
- Unaweza kuhitaji aina ya viti, misaada ya uhamiahi, au tiba

Shida zingine za Afya

. Aina nyingi za magonjwa ya muda mrefu au mfupi kama vile Ugonjwa wa Upungufu wa Umakini (ADHD), pumu, kisukari, kifafa, au magonjwa ya moyo. Magonjwa haya yanaathiri umakini, nguvu, nishati na kupunguza uwezo wa kufaulu shuleni.

Ulemavu Maalum wa Kujifunza

- Matatizo ya kusoma, kuandika, hesabu, au ujuzi mwingine wa kitaaluma
- Mtoto ana akili ya wastani lakini anatatizika kujifunza sehemu zingine

Ulemavu wa Kuongea ama Lugha

- Matatizo ya kuongea vizuri, kuelewa au kutumia lugha, ama kutengeneza sauti
- Unajumuisha kigugumzi, shida ya matamshi, na kuchelewa kwa lugha
- Unaweza kuathiri ushiriki wa darasani na mawasiliano





Jeraha la Kiwewe la Ubongo

- Jereha la ubongo linalosababishwa na nguvu ya nje (k.m., ajali ya gari, kuanguka)
- Linaweza kuathiri kumbukumbu, kuzingatia, hisia, tabia, ama kujifunza
- Mara nyingi huitaji usaidizi wa kuendelea na kujifunza ujuzi tena

Ulemavu wa Macho kama vile Upofu

- Ukosefu wa uwezo wa kuona au upofu unaoathiri masomo
- Unaweza kuhitaji maandishi ya Braille, maandishi kufanya makubwa, au mwelekeo na kufunzwa kutembea
- Unaathiri kusoma, kuandika, na upatikanaji wa taarifa za kuona

Ucheleweshaji wa Maendeleo

Mbali na zile kategoria 13, kategoria ya “ucheleweshaji wa maendeleo” inaweza kutumika kwa watoto hadi miaka 9 wakati ambapo ulemavu fulani hauwezi tambulika lakini kuna ucheleweshaji mkubwa katika mojawapo au zaidi ya mambo haya:

- Maendeleo ya kimwili
- Maendeleo ya utambuzi
- Mawasiliano
- Maendeleo ya kijamii au kihisia
- Maendeleo yanayobadilika

Bado una maswali?

Ongea na meneja wa kesi wa mtoto wako, mwanasaikolojia wa shule, ama timu ya IEP.





Nawezaje kupata usaidizi kwa lugha yangu?

Omba huduma za mkalimani katika shule ya mtoto wako ama katika ofisi za wilaya ya shule. Omba maandishi yaliyotafsiriwa iwapo unahitaji. Taarifa zinazopatikana kwa wazazi wote katika wilaya ya shule zinafaa kupatikana kwako pia.

